

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA SONGEA



Tarehe; 09/03/2023

TANGAZO LA KAZI KWA MKATABA

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Songea anawatangazia Wananchi wote wenye sifa kuomba nafasi ya kazi za Mkataba kama inafuatavyo,

1. MSIMAMIZI WA UJENZI (NAFASI 1)

SIFA ZA MWOMBAJI

- Awe Mtanzania mwenye umri kati ya miaka 18-40
- Awe amehitimu elimu ya kidato cha Nne/Sita.
- Awe amehitimu Shahada ya Fani ya Uhandisi (Usanifu Majengo, Ukadiliriaji Majengo au Uhandisi Majengo) kutoka chuo kinachotambuliwa na Serikali.
- Awe amesajiliwa na Bodi husika.
- Awe mwenye uwezo wa kusimamia majengo ya Serikali (Mwombaji awe na uwezo wa kusimamia majengo ya sekta ya Afya, Utawala na Elimu kama vile Zahanati, Kituo cha Afya, Hospitali ya Wilaya na majengo ya Utawala na shule n.k)

MSAHARA NA POSHO

KWA KUZINGATIA VIWANGO VYA MSAHARA WA SERIKALI TGS E.1 NA POSHO YA MASAA YA ZIADA ISIYOZIDI SIKU 10 KWA MWEZI.

KAZI ZA KUFANYA

- i. Kuandaa mahitaji ya vifaa vya ujenzi vitakavyohitajika katika utekelezaji wa mradi kulingana na vipimo/mahitaji (specification) zilizopo kwenye mchoro
- ii. Kusimamia ufanisi wa mafundi viongozi na vibarua katika mradi.
- iii. Kuandaa na kuwasilisha mpango kazi wa kamati za usimamizi wa mradi kila wiki.

- iv. Kufanya vikao na kamati za utekelezaji wa mradi, kuandaa na kuwasilisha taarifa.
- v. Kuandaa tathimini ya kazi, hati ya malipo ya mafundi na kuitisha kwa Mhandisi Ujenzi kwa ajili ya malipo.
- vi. Kusimamia kazi zote za mradi (site) kulingana na maelekezo ya Mhandisi ujenzi, bajeti, ubora unaotakiwa na mpango kazi.
- vii. Kazi zingine zinazohusu mradi atakazopangiwa na Mhandisi Ujenzi.

MASHARTI YA JUMLA KWA WAOMBAJI WOTE


- a) Mwombaji awe Raia Tanzania mwenye umri usiozidi miaka 45
- b) Mwombaji lazima aambatanishe cheti cha kuzaliwa
- c) Mwombaji aambatanishe maelezo binafsi (CV) yanayojitosheleza (detailed CV) yenye anuani na namba ya simu pamoja na majina ya anuani za wadhamini (Referrees) watatu wa kuaminika
- d) Maombi yote yaambatane na nakala ya vyeti vya taaluma, nakala ya cheti cha kidato cha cha nne au sita kilicho halali, nakala ya vyeti vya kuhitimu mafunzo
- e) Mwombaji ambatanishe picha mbili ndogo (passport size) za hivi karibuni zenyre rangi kwa muono wa nyuma (Background)
- f) Testimonials, Provisional result, statement of result, hati ya matokeo ya kidato cha nne au sita hazitapokelewa.

MWISHO WA KUTUMA MAOMBI NI TAREHE 23 MACHI, 2023 saa 3 : 30 ALASIRI

Maombi yote yatumwe kwa anuani ifuatayo

Mkurugenzi Mtendaji,
Halmashauri ya Wilaya ya Songea,
1 Barabara ya Halmashauri
S.L.P 995,
57183, SONGEA.

Imetolewa na ,


 Neema M. Maghembe
MKURUGENZI MTENDAJI (W)
SONGEA

